**DISCOVERY NATIONAL EXAMINATIONS**
**KCPE COMPLIANT 2021**

# DARASA LA SABA

**DISCOVERY EXAMS**

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA:
## LUGHA

**Muda:Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandikia chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya majibu na usiikunje.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usikunje.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D.
   Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

19. Tumia kiambishi sahihi:-
    Darasa __ tajengwa kesho.
    A. i  B. u  C. li  D. ki

**Jibu sahihi ni C**
**Katika karatasi ya majibu**

9 [A] [B] [C] [D]  19 [A] [B] [C] [D]  29 [A] [B] [C] [D]  39 [A] [B] [C] [D]  49 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 19, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

*Discovery Education Publishers*

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

**Maswali 1 mpaka 15**

***Jaza pengo kwa kuchagua jibu bora zaidi.***

Kengele ___1___, wanafunzi wote walifuatana ___2___ kuelekea gwarideni. Ilikuwa kama ___3___ kila siku ya Ijumaa ___4___ pamoja kwa maombi. Wanafunzi wengine walisikika wakipiga ___5___ kuhusu matukio ya ___6___ nzima iliyopita.

Kila darasa lilijipanga ___7___ safu zao wakimsubiri mwalimu kwa ___8___ kufika . Mara tu ___9___, maskauti waliongoza ___10___ bendera na kuimba wimbo wa taifa.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. imelia | B. ilipolia | C. inagongwa | D. ilichapwa |
| 2. | A. hobelahobela | B. kukuru kakara | C. unyounyo | D. juu chini |
| 3. | A. ibada | B. mazoea | C. mchezo | D. bwerere |
| 4. | A. kuishi | B. kujumuika | C. kuingia | D. kwenda |
| 5. | A. sakata | B. kelele | C. fujo | D. soga |
| 6. | A. wiki | B. juma | C. mwaka | D. mwezi |
| 7. | A. ndani ya | B. karibu | C. katika | D. kwa |
| 8. | A. moyo mkunjufu | B. hali na mali | C. jino na ukucha | D. hamu na ghamu |
| 9. | A. alipofikia | B. alipokaribia | C. alipowadia | D. aliporejea |
| 10. | A. kutweka | B. kupandiza | C. kutwika | D. kuinua |

Siku hizi ___11___ wanahadaiwa na ___12___ na utamaduni wa ___13___. Wengi wao huiga chochote kinachotoka ___14___. Ukweli wa methali kiingiacho mjini si ___15___ umepataka kudhihirika.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. wazee | B. vijana | C. wasichana | D. wakongwe |
| 12. | A. mila | B. miiko | C. tabia | D. hadithi |
| 13. | A. Mashariki | B. Kaskazini | C. Kusini | D. Magharibi |
| 14. | A. Unguja | B. Uhabeshi | C. Ughaibuni | D. Uganda |
| 15. | A. haramu | B. halali | C. chochote | D. lolote |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Toa jibu mwafaka kwa salamu hii.

Makiwa!

A. binuru

B. tunayo

C. alamsiki

D. inshallah

17. Kanusha:

Ungefika mapema ungempata daktari.

A. Ungalifika mapema ungalimpata daktari

B. Ungelifika mapema ungelimpata daktari

C. Usingefika mapema usingempata daktari

D. Usingalifika mapema usingalimpata daktari

18. Tegua kitendawili:

Hutembea juu ya miba ingawa hachomwi.

A. mkuki

B. nanasi

C. ndege

D. ulimi

19. Chagua sentensi inayoonyesha matumizi sahihi ya po ya wakati.

A. Anapochezea pana shimo kubwa

B. Pole pole ndio mwendo

C. Alipokaa ndipo pao

D. Aliponitafuta alinipata sokoni

20. Sentensi gani isiyobainisha matumizi ya neno panda?

A. kukwea mti au mlima

B. kuweka mbegu au miche ardhini ili imee

C. mnyama mkubwa wa nchi zenye baridi

D. kifaa cha watoto cha kuulia ndege

21. Chagua jibu mwafaka la kusisitiza:

Vitendo ____________ ndivyo vilivyowafanya washtakiwe.

A. hivyo hivyo

B. hivo hivo

C. vivyo hivyo

D. hicho hicho

22. Tunasema mweusi kama makaa, vilevile mwepesi kama:-

A. mboga

B. paa

C. mawingu

D. hewa

23. Mtoto wa nyuki ni jana. Je, mtoto wa chungu huitwa ____

A. nirihi

B. kiwavi

C. kiluwiluwi

D. kwida

24. Nini maana ya usemi kula mwata?

A. Kuwa na shida au kuteseka

B. kutumia pesa au mali vibaya

C. kuwa na maisha marefu

D. kula pamoja na marafiki

25. Kamilisha methali:

Mgonjwa haulizwi _______

A. dawa

B. daktari

C. matibabu

D. hospitali

26. Chagua jawabu linaloonyesha kinyume cha jinsia kwa usahihi:-

A. Beberu - mbuzi

B. Jimbi - koo

C. Mjomba - mtwana

D. Malkia - tembe

27. Mwanafunzi huyu ni mtiifu. Maneno yalipopigiwa kistari yanaonyesha ____

A. kiashiria na kivumishi sifa

B. kielezi na kivumishi

C. kiashiria na kimilikishi

D. kihusishi na kielezi

28. Ndugu wa kike na wa kiume huitwa:-

A. mpwa

B. harimu

C. umbu

D. mkoi

29. Chagua sentensi inayoonyesha matumizi ya karibu ya idadi.

A. mtihani wa kitaifa u karibu

B. karibu gari letu litumbukie mtoni

C. kwao ni karibu na msitu

D. walikuwa karibu abiria watano garini

30. Chagua kiunganishi sahihi kukamilisha sentensi:-

Mzee Omari ni tajiri ______ hana watoto wa kurithi mali yake.

A. isipokuwa

B. ingawa

C. ilhali

D. wala

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Uchumi ndio uti wa mgongo wa taifa lolote lile. Huimarisha maisha ya wananchi na ya kijamii.

Kunao uhusiano mkubwa baina ya ukuaji wa uchumi na mfumo wa kisiasa unaoshikiliwa na viongozi wa taifa husika. Kadiri nchi inavyoongozwa na wanasiasa wenye viwango vya juu vya maadili na elimu, ndivyo nchi inavyofikia ufanisi mkubwa wa kiuchumi.

Wasomi wanasema, utafiti unaonyesha kuwa viongozi fisadi wanapoongoza taifa husika, huathirika moja kwa moja kiuchumi. Hii ni kwa sababu rasilimali za nchi hunufaisha wachache walio katika tabaka la uongozi. Mfumo wa kisiasa ukipigana na suala la ufisadi, uchumi huimarika zaidi.

Nchi yetu inaathirika zaidi kutokana na uongozi wa viongozi tofauti. Mpaka sasa, adui mkubwa wa maendeleo ya nchi yetu ni ufisadi. Dawa mujarabu ya kuimarisha uchumi wetu ni kupigana na uongozi mbaya, kwa kuwachagua viongozi waliostaarabika ili janga hili la kuhodhi na kufuja mali ya umma lipate kuangamizwa kabisa.

Elimu hupelekea watu kuwachagua viongozi bora bila kuangalia tabaka, ukabila, dini au rangi. Aidha elimu husaidia kufanikisha utafiti na kupata suluhisho la matatizo kwenye nyanja za afya, kilimo, biashara na mawasiliano.

31. Uchumi ndio uti wa mgongo wa taifa ndio kumaanisha?

A. Ndio mti unaozaa matunda ya maendeleo

B. Ni nguzo kubwa ya maendeleo nchini

C. Ndio mgongo wa taifa

D. Husimamia uchumi wetu wa taifa

32. Nyanja gani zilizotajwa zinazoimarishwa na uchumi bora

A. kijamii na kiuchumi

B. kisiasa na kijamii

C. kijamii na kimaadili

D. kisiasa na kijamii

33. Kunao uhusiano gani katika taifa ili maendeleo yapatikane?

A. Uhusiano wa mataifa ya nje

B. Uhusiano wa familia katika nchi

C. Uhusiano wa viongozi na ukuaji wa uchumi

D. Uhusiano wa ufisadi na uchumi

34. Kadiri viongozi fisadi wanavyoongoza nchi ndivyo ______

A. hudorora kiuchumi

B. huimarika kiuchumi

C. hukua kiuchumi

D. huinuka kiuchumi

35. Rasilimali za nchi ________ na viongozi wabaya.

A. huvunjwa

B. huundwa

C. huvujwa

D. hufujwa

36. Ni jambo lipi analotaja mwandishi kuwa linasaidia kuwachagua viongozi bora?

A. Tabaka

B. Elimu

C. Ukabila

D. Uchumi

37. Kuchagua viongozi bila kuangalia kabila, dini au rangi huitwa?

A. Uhuru

B. Ukweli

C. Demokrasia

D. Maendeleo

38. Habari hii inahimiza?

A. Kukoza uchumi

B. Utaifa wa wananchi

C. Kuchagua viongozi

D. Ukabila wa wananchi

39. Dawa mujarabu kulingana na mwandishi ya kuimarisha taifa letu ni:-

A. kuchagua viongozi vijana

B. kuzingatia ukabila katika uchaguzi

C. kuchagua viongozi fisadi

D. kupiga vita uongozi mbaya

40. Kichwa mwafaka kwa taarifa uliyoisoma chaweza kuwa:-

A. uongozi bora

B. uchumi wa nchi

C. uchaguzi ujao

D. viongozi fisadi

*__Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50.__*

Shule ya msingi ya Nyota,
Sanduku la posta 44,
Kijijini

28/01/2016

Mpendwa Rehema,

Pokea salamu zangu belele mithili ya mchanga kwenye ufuo wa bahari. U hali gani msena? Natumai u buheri wa afya na mzima kama ngarange za msonobari. Nasadiki kuwa Mola amezidi kukubariki kwa afya na siha za tembo. Mimi sijambo. Maisha yanazidi kuninyooka. Mambo hapa ni bambam bila shari wala swali.

Mwandani Rehema, nachukua fursa hii kukuarifu kuwa nimejiunga na darasa la saba katika shule ya Elimu Bora. Wavyele wangu walionelea wanihamishie shule hii ya bweni; ili kuimarisha masomo yangu na kuyafikia malengo yangu ya kupasi mtihani wangu wa kitaifa.

Ninayo matumaini mengi kama tai kuwa nitafua dafu. Ari yangu kubwa ni kujizolea alama zaidi ya mia nne kabla ya kujiunga na darasa la nane hapo mwakani. Ninazidi kuuma meno au kushikilia uzi ili kutimiza ndoto yangu. Nawakamia na kuwakakamia walimu wangu kwa maswali belele chembilecho <u>mficha uchi hazai</u>. Kudurusu na kubukua matopa ya vitabu ni jambo ninalolishikilia kwa moyo wa dhati; bila kuchoka. Wanaocheza ngoma goya nimewaambaa kama shetani. Natumai waelewa kuwa nazi mbovu harabu ya nzima.

Msiri Rehema, nakushika sikio; ufanye bidii masomoni kwani bidii hulipa. Jitanibu na walio watepetevu ili kuboresha aushi yako ya baadaye. Waheshimu wakuu wako, bila kusahau kuwa Mungu yupo na baraka zake ni belele. Nakomea hapo kwa sasa. Wasabahi wavyele wako, na wote wanaonifahamu. Natumai kuupokea waraka wa majibu yako hivi karibuni. Asante mwandani

Mimi wako wa kufa kuzikana
**Taabu Bahati.**

41. Taarifa uliyoisoma ni mfano wa:-
A. barua rasmi
B. barua ya kidugu
C. barua ya kiofisi
D. hotuba rasmi

42. Mwandishi wa barua hii ni?
A. Mwanafunzi wa shule ya Nyota
B. Mwanafunzi wa shule ya Kijijini
C. Mwanafunzi wa shule ya Bweni
D. Mwanafunzi wa shule ya Mwandani

43. Mambo yakikwendea bambam na shwari ndio kusema yanakuendea ____
A. mrama
B. pepe
C. tenge
D. vyema

44. Ni methali gani inayotuhimiza tusifiche shida zetu?
A. Nazi bovu harabu ya nzima
B. Baraka za Mungu ni belele
C. Mficha uchi hazai
D. Kucheza ngoma goya darasani

45. Rehema anashauriwa:
A. kujitanibu na walio watepetevu
B. kuogopa walimu na kuwaheshimu
C. kuwapenda wanaocheza ngoma goya
D. kujiunga na shule ya bweni ili afaulu

46. Tunasema barua ni nusu ya:-
A. kupigana
B. kuandika
C. kuonana
D. kupendana

47. Taabu anamsihi Rehema kuwaheshimu wakubwa wake kama vile:-
A. walimu na wazazi
B. wanafunzi na walimu
C. wandani na wavyele
D. viranja na wanafunzi

48. Rafiki wa kufa kuzikana ni rafiki:-
A. asiyetegemewa
B. wa kuaminika na kutegemewa
C. anayeongoza darasani
D. wa kutoka utotoni

49. Madhumuni hasa ya kuuandika waraka huu ni:-
A. kumwomba Rehema awachane na marafiki watepetevu
B. kumkaribisha Rehema katika shule ya bweni
C. kumshika sikio mwandani wake masomoni
D. kumwarifu mwandani kuwa alijiunga na shule ya bweni

50. Msemo kucheza ngoma goya una maana gani?
A. Kufanya bidii za mchwa
B. Kushirikiana katika masomo shuleni
C. Kufanya kazi za bure
D. Kuwaheshimu wakubwa wako.